OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI MGOLOLO
S.L.P 63
MGOLOLO-MUFINDI

30 MARCH 2022

NAMBA ZA SIMU
Mkuu wa shule 0755810913
Makamu mkuu wa shule 0763448059

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi
……
S.L.P……
……

YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MGOLOLO HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2022</u>

1.0 Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari Mgololo mwaka 2022 tahasusi ya .....

1.1 Shule ya Sekondari Mgololo ipo umbali wa kilometa 90 Kusini mwa mji wa Mafinga. Usafiri wa basi kutoka mjini MAFINGA unapatikana katika kituo cha mabasi MAFINGA kwa nauli ya tsh.7,000/= kuanzia saa 3:30 asubuhi hadi saa 6.30 mchana. Unaweza kufika Mgololo kupitia mji wa MAKAMBAKO,stand ya zamani ambapo utapata usafiri wa basi na noa kwa Tsh.5,000= kuanzia saa 2.30asubuhi hadi saa 10.30 jioni

1.2. Muhula wa masomo unaanza **SEPTEMBA 2022** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe 05.09.2022 tayari kwa kuanza masomo. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **10.09.2022.**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 . Sare ya shule

- Sare ya shule hii ni Suti ya koti mikono mirefu rangi blue nyeusi (dark blue), suruali zishonwe vizuri, ziwe na marinda mawili na zisiwe nyembamba chini (PIMA INCH 16-18), ziwe na turn up na zivaliwe kiunoni kwa mkanda mweusi wa ngozi
- Mashati mawili meupe ya mikono mirefu yenye mfuko mmoja upande wa kushoto

- Tai rangi ya blue nyeusi (dark blue).
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba visivyo na urembo
- Soksi nyeusi jozi mbili.
- T-shirt mbili (form six) rangi ya kijivu zenye nembo ya shule (zitapatikana shuleni kwa shilingi elfu kumi na tano kila tisheti
- Jozi moja ya nguo za michezo. (bukta ya blue na T-shirt ya blue).
- Track suit moja ya rangi ya blue
- Nguo za kushindia (shamba dress) suruali mbili rangi ya kaki.
- Sweta la shule rangi ya blue nyeusi(dark blue)
- Pull neck nyeusi.

NB: *HAURUHUSIWI KUJA NA NGUO NYINGINE YEYOTE ISIYO SARE YA SHULE.*

2.2. Ada na michango ya shule

(a) . Ada ya shule ni shilingi elfu sabini (70,000/=) kwa mwaka.Unaweza kulipa yote au kwa awamu mbili,yaani elfu thelathini na tano tu kwa kila muhula(35,000/=) mwanzoni mwa kila muhula au zote mwanzoni mwa mwaka kwa maramoja. Fedha hizo za Ada zilipwe kwa kupitia **A/C Na.60201200099,** Jina la akaunti **Mgololo secondary school** katika tawi lolote la NMB na uwasilishe risiti ya kulipia(**Bank Pay in Slip**) kwa mhasibu pindi ufikapo shuleni (**Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).**

(b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

S/NA	MALIPO	KIASI
(i)	TAALUMA	20,000/=
(ii)	TAHADHARI (haitarejeshwa)	5,000/=
(iii)	KITAMBULISHO	6,000/=
(iv)	KUWALIPA WAPISHI, WALINZI NA VIBARUA WENGINE	30,000/=
(v)	UKARABATI WA SAMANI	15,000/=
(vi)	NEMBO YA SHULE	2,000/=
(vii)	MITIHANI YA KUJIPIMA	20,000/=
(viii)	MITIHANI WA ANNUAL MKOA	10,000/=
	JUMLA	**108,000/=**

JUMLA KUU YA ADA NA MICHANGO NI SHILINGI 178,000/=

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni :-

a. Rimu ya karatasi 2 (kwa mwaka) muhula wa kwanza limu moja na muhula wa pili limu moja

Michango yote ambayo jumla yake ni tsh. 108,000= ilipwe kwa mara moja kupitia akaunti na**. 60210050119**, Jina la akaunti ni EK MGOLOLO SEKONDARI, Benk ya NMB.

b. Shuka mbili za rangi, ya pinki 1 na bluu bahari.1(light blue), blanketi 1, chandarua 1, mabuti ya mvua gamboots), net 1ya mbu ya mviringo.
c. Tochi au taa ya solar(solata), mwavuli.
d. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko

e. Godoro la futi mbili na nusu lenye **unene wa inchi 4, mto wenye foronya mbili za rangi ya pink na blue bahari.**
f. Uwe na sanduku linalofunga vizuri kwaajili ya kuhifadhi nguo na vitu vyako.
g. Vyombo vya chakula kama sahani,bakuli, kontena, kijiko, jagi la maji ya kunywa na kikombe.
h. Kwanja 1, jembe 1 lenye mpini, panga 1, reki 1, mifagio ya ndani(soft broom 1), na mopper 1
i. Scientific calculator
j. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
k. Madaftari 10 makubwa ya kutosha mahitaji yako ya masomo.(counter books)
l. Dissecting kit kwa wanaosoma BIOLOGY

m. Kamusi (dictionary) ya kiingereza-kiingereza.
n. Cheti cha matokeo kidato cha nne (Result slip)

o. Faili mbili (spring files) kwaajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.
P. STOP WATCH kwaajili ya masomo kwa vitendo

AFYA/MATIBABU
Mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya au fedha Tsh. Elfu tano kwaajili ya kujiunga na bima ya afya iliyoboreshwa (CHIF). Pamoja na kuwa na kadi ya bima unatakiwa kuja na fedha Tsh.elfu kumi kwaajili ya usafiri wa kutoka shuleni kwenda Kituo cha afya ambacho kipo kilometa tatu kutoka shule ilipo. Endapo mwanafunzi atahitajika matibabu zaidi mzazi au mlezi atajulishwa na kuwajibika kumpeleka kwenye matibabu zaidi, hii ni pamoja na kununua dawa ambazo hazitakuwepo katika kituo cha afya.

HUDUMA ZA KIBENKI
Ili kufanikisha na kurahisisha utumaji wa fedha za matumizi ya mwanafunzi , mzazi/mlezi hakikisha unamfungulia mwanao akaunti katika benk za NMB, na CRDB na kama utashindwa kumfungulia akaunti aje na fedha tsh.10,000, picha mbili za passport kwaajili ya kufungulia akaunt hiyo shuleni kwani wahudumu wa NMB na CRDB hufika shuleni kutoa huduma hiyo.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

A: HESHIMA

Katika kuzingatia heshima kila mwanafunzi anapaswa kuzingatia yafuatayo;

1. mwanafunzi asimame anapomsalimia mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri.
2. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia lugha mbaya wakati wowote, kati yao wenyewe, kwa walimu na kwa watu wengine.
3. Mwanafunzi awaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
4. Mwanafunzi aoneshe moyo wa kusaidia na kushirikiana katika kazi.
5. Mwanafunzi aheshimu na kuthamini kazi za aina zote zinazofanyika shuleni.
6. Ni marufuku kwa mwanafunzi kufanya mambo yafuatayo;
    a) Kuvuta sigara
    b) Kufuga kucha ndefu na kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi
    c) Kufuga ndevu
    d) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima
    e) Kugombana
7. Mwanafunzi atii na kuitika wito kwa kukimbia kila anaposikia wito kwa kengele au mwalimu.

8. Mwanafunzi aheshimu Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Taifa na fedha ya Taifa. Pia ashiriki kupandisha bendera ya Taifa katika siku husika.
9. Mwanafunzi aheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, ofisi za shule mali binafsi na mali ya Umma.
10. Mwanafunzi asimame katika mstari wakati wa kupokea huduma.
11. Mwanafunzi anyooshe mkono na asimame anapouliza na kujibu maswali.
12. Mwanafunzi akae kimya wakati wote awapo darasani na asitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi yeyote wa darasa lake.
13. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja shuleni na simu au vifaa vya muziki kama redio, headphone, computer nk.

B: MAHUDHURIO

1. Mwanafunzi ahudhurie shule kwa muda wote wa masomo
2. Mwanafunzi ahudhurie vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa
3. Mwanafunzi ahudhurie na ashiriki kazi zote za mikono
4. Mwanafunzi ahudhurie mikutano yote halali ya shule kama kupandisha Bendera ya Taifa, Baraza na mikusanyiko mingine ambayo ni rasmi.

C: MAANDALIO YA JIONI

1. Ni lazima kila mwanafunzi ashiriki maandalio ya jioni
2. Ni lazima kila mwanafunzi kufanya kazi alizopewa na mwalimu wakati wa maandalio ya jioni
3. Ni lazima kila mwanafunzi kuzingatia muda wa kuanza na kumaliza maandalio ya jioni.

D: KUWAHI

1. Mwanafunzi athamini muda
2. Mwanafunzi awahi shuleni na kuzingatia ratiba ya kila siku ya shule
3. Mwanafunzi aitikie wito wa dharura kwa kukimbia kule anakotakiwa
4. Mwanafunzi atii kengele
5. Mwanafunzi afike shuleni tarehe iliyopangwa na aondoke tarehe iliyopangwa na uongozi wa shule.

E: MIPAKA YA SHULE

1. Ni marufuku mwanafunzi kutembea sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu:
    a) Chumba cha mwalimu
    b) Ofisi ya mwalimu
    c) Maabara
    d) Jikoni
    e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
2. Ni marufuku kabisa kwa mwanafunzi kutembelea au kuonekana katika sehemu zifuatazo;
    a) Vilabu vya pombe
    b) Majumba ya starehe
    c) Nyumba za kufikia wageni
3. Ni marufuku kwa mwanafunzi wa bweni/hosteli kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa maalumu na kibali maalumu.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- Ruhusa ya kutokuwepo shuleni kwa siku moja au zaidi itatolewa na mkuu wa shule, makamu mkuu wa shule au mwalimu aliyekasimiwa madaraka.
- Mwombezi wa ruhusu anayeruhusiwa kukuombea ruhusa ni mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni na siyo mtu mwingine yeyote.
- Lugha rasmi unayotakiwa kutumia kwa mawasiliano shuleni ni kiingereza tu

- Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuchezea vifaa au miundombinu yoyote ya umeme kama swichi, socket, taa, mita nk. Ni kosa kubwa kujiunganishia nyaya za umeme kwa matumizi yeyote yasiyo rasmi. Ukikamatwa utafukuzwa shule mara moja au kulipa roll ya wire ya 1.5mm mita 100 pamoja na gharama za fundi.
- Huruhusiwi kutumia mishuma na badala yake tumia tochi au solata endapo umeme utakatika.
- Mzazi au mlezi anaweza kukutembelea jumapili ya kwanza ya mwezi kuanzia saa nne asubuhi mpaka saa kumi jioni.
- Mwanafunzi anatakiwa kufika na kivuli (photocopy) cha cheti cha kuzaliwa

3. **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
(vii) Kufuga ndevu
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(ix) Uvutaji wa sigara.
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale. yanayovunja sheria za nchi;
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jina
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

NYAULINGO J.M
MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
MGOLOLO SEC SCHOOL
P. O. Box 63, MGOLOLO IRINGA
Date:.....Sign.....

KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI

A. MWANAFUNZI NA WAZAZI/WALEZI WAKE

i. Jina la mwanafunzi.....

ii.Tarehe ya kuzaliwa.....mahali.....

iii.Jina la baba.....yu hai/amefariki.....

iv. Mahali anakoishi;

Kijiji/Mji.....kata.....tarafa.....

v. Kazi ya baba.....

vi. Anwani yake.....simu.....

vii. Jina la mama.....yu hai/amefariki.....

viii. Mahali anakoishi;

Kijiji/Mji.....kata.....tarafa.....

ix. Kazi ya mama.....

x. Anwani yake.....simu.....

xi. Jina la mlezi.....

xii. Mahali anakoishi;

Kijiji/Mji.....kata.....tarafa.....

xiii. Anwani yake.....simu.....

B. NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

NA	JINA	UHUSIANO	NA.YA SIMU/ANWANI
1			
2			
3			
4			
5			
6			

C. AHADI YA KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE(MWANAFUNZI)

Mimi.....naahidi kufuata sheria,kanuni na taratibu za shule hii na kutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na uongozi wa shule wakati wote nitakaokuwa ndani na nje ya shule.Sitajihusisha na migomo,fujo wala makosa ya jinai.

Sahihi.....tarehe.....

D. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi.....ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyeweka ahadi hapo juu,naahidi kumpatia ada ya shule,michango na mahitaji yote yanayotakiwa kujiunga na shule hii.

Sahihi.....tarehe.....

PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MUFINDI DISTRICT COUNCIL
MGOLOLO SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officers in a recognize Hospital in respect of all new entrants to Mgololo Secondary School.

Full name.....
Age.....

1. Blood comment (Red&White).....
2. Urine examination.....
3. Stool examination.....
4. Syphilis test.....
5. T.B test.....
6. Ear test.....
7. Eye test.....
8. Speen.....
9. Abdominal.....
10. Additional information or any other physical, hereditary or infectious disease:
    .....
    .....
    .....

    Treatment after examination:
    .....
    .....

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue for further education.
Signature.....
Designation.....
Station.....
(official stamp).....
Date.....

NB:Fomu hii ijazwe na Mganga katika hospitali inayotambulika na Serikali.

ORODHA YA VITABU AMBAVYO MZAZI ANAWEZA KUVINUNUA KWA AJILI YA MWANAO KUJISOMEA YEYE BINAFSI.

a. Chemistry

i). Advanced level organic chemistry by APE network 2012
ii). A' level secondary Education chemistry practical
iii). Advanced inorganic chemistry volume I and II by S. CHAND
iv). Environmental chemistry and pollution control by S.CHAND
v). Essential physical chemistry by S. CHAND
vi). Selected topics in inorganic chemistry by Wahid U. Malik et al
vii). Organic chemistry by S.CHAND

b. Physics

i). A' level physics 4th edition. By Roger Muncaster
ii). S. Chand's principle of physics for class xi
iii). S. Chand's principle of physics for class xii
iv). Nelkon & Parker 7th edn
v). University physics
vi). Calculation for A' level physics
vii). Engineering physics

c. Biology

i). CJ CLEGG with DG MACKEAN (2000) Advanced Biology principles and Application 2nd Ed, Hodder Murray London
ii). Sylvia S Mader (1996), Biology (5th Ed) Wm C. Brown publisher London
iii). DJ Taylor et al (1997), BIOLOGICAL SCIENCE, Cambridge university press – New York.
iv). MBV Roberts (1986), Biology A functional Approach (4th Ed)
v). Ann Fullick et al (2011), A level Biology, students Book, Longman.

d. General studies

i). General studies for A' level certificate form v (by. RICHARD R MBALASE)
ii). General studies for A' level certificate form vi. (By RICHARD R. MBALASE)

e. Geography

i). Practical geography Alive (by Zisti)
- Map Reading, photography Interpretation, Field Research, Statistics, and Survey Illustrated(by Ellias Anthony Mkoko)
- Affordable Edition for secondary and High school learners (kot publishers)

ii). A comprehensive approach to physical geography (by D.T. Msabila)
iii). Human and Economical Geography (by Gillan C. Morgan)
iv). Soil and Climatology (by Zisti)

f. Mathematics

i). Pure mathematics 1 (by J.K Backhouse)
ii). Pure mathematics 2 (by J.K Backhouse)
iii). Pure mathematics 1 (L. Bostock and Chandler)
iv). Advanced mathematics, (Tranter CJ)
v). S. Chand's mathematics volume 1, Fourth Edition (by H.K Dass and RAMA VERMA)
vi). S. Chand's mathematics volume 2, Fourth Edition (by H.K Dass and RAMA VERMA)
vii). Potics in Algebra (by DR. P.N.ARORA)